HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI
FURSA ZA UWEKEZAJI ZILIZOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI

1. SEKTA YA ARDHI NA MALIASILI

S/N	SEKTA	FURSA ZILIZOPO	KILICHOFANYIKA HADI SASA	KITAKACHOFANYIKA
i.	ARDHI	Ardhi iliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda katika kata zote 21 za Halmashauri ya Wilaya.	Barua maelekezo kwa watendaji wa kata kutenga maeneo ya uwekezaji zimeandikwa kwa kata zote 21. Hadi sasa kata tatu (3) za Kwamsisi, Kang'ata na Segera zimethibitisha uwepo wa eneo hilo.	Ufuatiliaji kwenye kata zilizosalia unaendelea. Aidha upimaji wa maeneo yanayotolewa utaenda sambamba na upatikanaji wa maeneo hayo ili kuandaa hati miliki.
		Ardhi iliyotengwa kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji jumla ya Hekta 68,134 sawa na ekari 170,335 (24% ya eneo lote la Halmashauri.	Halmashauri inafanya ukaguzi wa mashamba makubwa yote yenye Hati nay ale yasiykuwa na Hati ili kuona uendelezaji wa mashamba hayo. Hadi sasa jumla ya mashamba 10 yamekaguliwa na hatua kisheria zinaendelea ili kurejesha ardhi hiyo kwa wawekezaji wengine.	Hatua inayofuata sasa ni kutoa notisi za kuwahimiza kuendeleza mashamba hayo katika kipindi cha siku 90, hatimaye notisi za kusudio la kuwafutia hati miliki zitafuata kwa mujibu wa sheria na mashamba hayo kupewa wawekezaji wengine.
		Uendelezaji miji ya Kabuku, Mkata na Segera	Halmshauri ya Wilaya kwa kushirikiana na jamii ipo katika hatua ya kutambua makampuni yaliyosajiriwa kufanya kazi za mipango miji na upimaji yenye uwezo wa kushirikiana na Halamshauri ili kurasimisha makazi na kupima viwanja vya matumizi mbalimbali katika miji ya Mkata, Kabuku na Segera. Tayari kampuni tatu zimewasilisha maombi na tupo katika hatua ya mwisho ili kuanza kazi.	Halmashauri itahakikisha kwamba maeneo yatakayotengwa na kupimwa ni pamoja na uwekezaji wa viwanda, shule, masoko, maegesho, vituo vya magari, viwanja vya kibaishara na makazi
		Ujenzi wa soko la Kimataifa la matunda na mabogamboga Segera	Eneo limeainishwa lenye ukubwa wa ekari 100 limetengwa, ambapo hadi sasa ni ekari 40 tu zimepimwa. Fidia kwa wamiliki bado haijafanyika.	Juhidi zinzoendelea hadi sasa ni kutafuta mwekezaji atakayeshirikiana na Halmashauri, serikali ya kijiji na wailiki wa maeneo hayo ili mradi huu uweze kuanza.
	MISITU NA NYUKI	Uwepo wa misitu ya asili 81 inayomilikiwa na vijiji 17.	Halmashuri kwa kushirikiana na vijiji imeendelea kufanya doria za ulinzi wa misitu hii. Uwekezaji katika viwanda vya kuchakata mazao ya misitu unahitajika. Miti katika baadhi ya	Tumeanza utaratibu wa kukamilisha kamati za maliasili za vijiji, mipango ya usimamizi wa misitu ikijumuisha mipango ya uvunaji endelevu wa

			misitu hii imefikia kiwango cha kuvunwa magogo, mbao na mkaa. Aidha uwekezaji katika sekta ya ufugaji nyuki katika misitu hii unahitajika.	mazao ya misitu.

2.0: SEKTA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA MIFUGO.

Na.	Fursa zilizopo	Kilichofanyika hadi sasa	kitakachofanyika
1	Eneo la kilimo kwa mazao yote ya nafaka, mboga mboga na matunda	Halmashauri ina eneo linalofaa kwa kilimo cha aina yote lenye ukubea wa hekta 287,966	Kupanua wigo kwa wananchi kuendeleza kilimo cha mazao ya aina zote (Chakula na Biashara). Kuna ardhi yenye ukubwa wa takribani hekta 140,000 bado hazijatumika
2	Kuwepo kwa eneo la umwagiliaji	Halmashauri ya wilaya ina eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji hekta 5,596 na zinazotumika ni hekta 50 tu	Uwepo wa programme ya DIDF eneo la Jambe – Kwadoya na mto pangani usiokauka kwa kipindi chote cha mwaka
3	Udongo bora na pekee duniani kwa Kilimo cha mazao ya matunda (embe, chungwa, ndizi na nanasi)	Wawekezaji binafsi wazalendo na wageni wameanza kilimo cha Embe Kabuku, Chungwa Kwamgwe na Ndizi Kwamsisi	Kukaribisha wawekezaji wengi zaidi ili kuendelea kuwekeza kilimo cha mazao ya matunda kutokana na udongo mzuri kwa mazao ya matunda
4	Eneo la malisho ya mifugo	Halmashauri ya wilaya ina eneo la Hekta 367,530 linalofaa kwa malisho ya aina zote za mifugo wapatao 200,000 na ambalo bado halijatumika	Kubinafsisha kwa wekezaji wa ranchi za mifugo

3.0: SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA

Na	Sekta	Eneo la Uwekezaji (Mahali na Ukubwa)	Hali/ Hatua iliyofikiwa	Maoni
1	VIWANDA	Eneo lipo Segera na lina ukubwa wa ekari tano na linategemewa kujenga kiwanda cha juisi ya matunda	Kulipa fidia na Upimaji	
		Eneo lipo Kabuku Mjini lina ukubwa wa ekeri 50 walipewa JKT Mgambo ili wajenge Kiwanda cha kusindika matunda lakini walishindwa na sasa limerudishwa kwa serikali ya Kijiji	Upimaji	Eneo halina fidia kwa sababu lilikuwa wazi kwa kipindi cha miaka saba sasa.
		(i)Kiwanda Cha Unga Wa Mahindi, eneo lipo kwachaga kijiji cha Tuliani, lipo kwa ajili ya ujenzi Kiwanda cha unga wa mahindi. Lina ukubwa wa ekari 10	eneo limeshatambuliwa na liko tayari kwa ajili ya uwekezaji	Wanakaribishwa wawekezaji ili kufanya uwekezaji shirikishi

2	MASOKO	Eneo lipo Segera na lina ukubwa wa hekta 367.2 sawa na Ekari 901	Kulipa fidia na Upimaji	Wanakaribishwa wawekezaji kujenga miundombinu ya kibiashra kama vile viwanda vya usindikaji wa matunda, Maghala, Maeneo ya kupumzikia wageni, mabenki,, maduka makubwa, Hoteli, sehemu za burudani, na nyumba za kuishi

4.0 SEKTA YA UTAMADUNI NA UTALII.

NA	JINA LA KIVUTIO	SIFA	MAHALI ILIPO
1	Pango la bwana heri	Alijificha mfalme aliyeitwa Saidi Bwanaheri mwaka 1942 wakati wa mapigano ya vita vya pili vya Dunia hivyo pango hilo likapata umaarufu	Kijiji cha Kwedikabu
2	Msitu wa Kwamsisi	Msitu huu ni chanzo cha maji pia una samaki aina ya Kambale wasiovuliwa, miti aina Mikangazi mikubwa na isiyovunwa na maarufu kwa shughuli za matambiko.	Kijiji cha Kwamsisi
3	Kaburi la Kibanga	Huyu ni mwana Handeni aliyepigania uhuru wa wananchi wa Handeni wakati wa ukoloni kwa kumpiga mkoloni aliyekuwa anawatesa wananchi bila sababu	Kijiji cha Kwachaga
4	Bonde lenye mapango katika msitu wa mlima Kofi kwa Mang'weng'we	Ndege haweza kuruka kwa kuvuka bonde/pango hilo kwani akivuka lazima afe na inasemeka bonde limejaa mizoga kutokana na ndege kuvuka	Kijiji cha Chanika Kofi
5	Mlima kilimamzinga	Jina la mlima huu limetokana na mapigano ya kivita kati ya Waingereza na Wajerumani ambapo kulikuwa na milipuko ya mizinga juu ya mlima huo na pia juu mlima huo kuna jiwe linalofanana na mzinga	Kijiji cha Kilimamzinga
6	Ngoma ya asili ya wazigua	Ngoma ya Selo, Mselego, Kajanja, Ukala, Vilangu, Machindi na Mbuji.	Maeneo mbalimbali ya Halmashauri
7	Vyakula vya asili	Hombo-mlenda, mbegu za maboga, matango, kweme, mnavu, ntula, cheluwe, mnkobo, mchunga/sunga, msokomela, nyago, bwando, ugali wa mtama na uwele na mlasi.	Maeneo mbalimbali ya Halmashauri.
8	Mavazi	Mgolole kwa wanawake na wanaume na kaniki kwa wanawake.	Maeneo malimbali ya Halmashauri
9	Nyumba za asili	Nyumba za msonge na tutu	Maeneo mbalimbali ya vijijini
10	Silaha za jadi	Mishale,gobore,mbigimbigi na nkumbayuwe	Maeneo mbalimbali mijini na vijijini
11	Njia ya watumwa wakati wa ukoloni	Kwedikwazu-Mbaula-Mailanga kuelekea Pangani.	Imeanzia Kwedikwazu.